

**OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA
SHULE YA SEKONDARI MWEGA, S.L.P 99 MIKUMI**

Tarehe: 18.12.2020

Kumb. Na. MWG/SS/ REG/2021/01
Mzazi /Mlezi wa
Malolo.

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA
SEKONDARI MWEGA KWA MWAKA WA MASOMO 2021**

Ninayo furaha kukuarifu kuwa mwanao

Amechaguliwa kijiunga na kidato cha **kwanza mwaka 2021** katika shule hii. Ninatumia fursa hii kumpongeza yeye na wewe mzazi/mlezi. Aidha ninamkaribisha sana hapa shulenii nikiamini kuwa ataendelea na juhudhi hizohizo kwa muda wote atakaokuwapo hapa.

Shule itafunguliwa **tarehe 11/01/2021**. Unatakiwa kumleta mwanao siku hiyo saa **1.30 asubuhi**.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-

1.0 Sare ya Shule:

(a) Wavulana:

- (i) Suruali(Cotton) ya damu ya mzee yenyе marinda manne mbele, mfuko mmoja wa nyuma na “belt hooks” za mkanda ziwe nyembamba za kawaida
- (ii) Shati jeupe la tetron lenye mikono mifupi (Tomato ni nzuri zaidi)
- (iii) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba (gidamu) na viwe havina kisigino kirefu
- (iv) Soksi nyeupe jozi mbili bila rangi yoyote au pambo lolote

Angalizo: Suruali za kubana (maarufu kama Modal) KAMWE HAZIRUHUSIWI. Mwanafunzi atakayekiuka atanyang’anywa na itachanwa. Aidha mshonee mwanao kwa kutumia kitambaa bora(Cotton)

(b) Wasichana:

- (i) Sketi ya damu mzee yenyе rinda kubwa mbele na nyuma, na marinda mawili mawili yanayotazama, belt isiwe pana sana. Sketi lazima ivuke magoti, vinginevyo haitakubalika.
 - (ii) Shati jeupe la tetron lenye mikono mifupi(Tomato ni nzuri zaidi)
 - (iii) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba(gidamu) visivyo na kisigino kirefu.
- (Angalizo: Viatu vya wazi (open shoes) na vyepesi (Bajaji) haviruhusiwi kabisa*
- (iv) Soksi nyeupe jozi mbili bila rangi yoyote au pambo lolote
 - (vi) **Hijabu:** Kwa wanaovaa hijab ifanane na shati la shule isiyo na urembo wowote. Ni marufuku kuvala hijab yenyе urembo wowote.

2.0 Vifaa vya darasani:

- (i) Madaftari makubwa (Counterbook 10) na Madogo 10 na Kalamu za wino za kutosha.
- (ii) Rula ya futi moja –nyeupe yenyе kuangaza na Mkebe (Mathematical set)
- (iii) Bunda moja la Karatasi (Ream 1 Ruled paper) kwa ajili ya kufanya Mitihani

NB: Bunda la karatasi kabidhi shulenii siku ya kuripoti

3.0 Mambo mengine muhimu:

- (a) Medical Examination form. Fomu hii ijazwe na Mganga mkuu wa hospitali ya serikali na ikabidhiwe kwa Makamu Mkuu wa shule siku ya kuripoti shulenii
- (b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo, makosa ya jinai, utii wa sheria na kanuni pamoa na kukubali kutekeleza maagizo mengine halali yatakayotolewa na shule.

NB: Fomu hizi na picha 2 lazima zikabidhiwe siku ya kuripoti shulenii bila kukosa.

Tanbihi: Tafadhalii soma kwa makini maelekezo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

SIKU YA KURIPOTI SHULENI MWANAFUNZI AJE NA MZAZI/ MLEZI WAKE, VINGINEVYO HATAPOKELEWA.

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE


Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu pamoja na OR- TAMISEMI kuhusu usimamizi wa Elimu nchini. Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatasitizwa na kufafanuliwa mara baada ya kuripoti shulenii:

- (a) Kucaa sare kamili ya shule wakati wote anapokuwa shulenii, anaposhiriki katika shughuli mbalimbali kama mikutano nje ya shule, safari za kielimu na popote pale anapoiwakilisha shule.
- (b) Heshima, utii na adabu kwa viongozi mbalimbali, walimu wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- (c) Mahudhurio mazuri darasani, katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
- (d) Kuwahi shulenii asubuhi na kufanya kazi za shule na nyingine utakazopewa.
- (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
- (f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule kwa ujumla.
- (g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- (h) **Ni marufuku kwa mwanafunzi kujipamba kama vile kupaka rangi kucha, kucaa bangili au hereni, kutinda nyusi, kuweka nywele dawa, kusuka, kunyoa kihuni, kufuga ndevu kulegeza suruali/sketi n.k.**
- (i) Ni marufuku kwa mwanafunzi kwenda kwenye nyumba za walimu/wafanyakazi bila ruhusa maalum.
- (j) Ni marufuku kwa mwanafunzi kuonekana kwenye kumbi za starehe, nyumba za kulala wageni n.k.
- (k) Ni marufuku kwa mwanafunzi kuandika kwenye vitabu vya shule , madawati, meza, viti, kuta n.k.
- (l) Ni marufuku kutumia lugha za matusi, kutoa maneno ya kashfa kwa walimu , wanafunzi au mtu mwingine ye yote yule.
- (m) Wanafunzi wote wanatakiwa kuishi kwa kupendana na kushirikiana kindugu.

Makosa yafuatayo yanaweza kusabisha mwanafunzi kufukuzwa shule:

- (a) Wizi
- (b) Uasherati na ushoga
- (c) Ubakaji
- (d) Ulevi wa aina yoyote na matumizi ya madawa ya kulevyaa kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubel n.k.
- (e) Kupigana au kupiga.
- (f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma au ya mwanafunzi mwingine.
- (g) Kudharau Bendera ya Taifa au Wimbo wa Taifa
- (h) Kuoa au kuolewa
- (i) Kupata mimba ndani na nje ya shule.
- (j) Kutoa mimba au kutia mimba
- (k) Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo, au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- (l) Kukataa adhabu halali kwa makusudi.
- (m) Mwanafunzi kukutwa na simu ya mkononi
- (n) Kutoroka shulenii wakati wa vipindi.
- (o) Kuchelewa kuripoti shulenii wakati wa kufungua shule.

Nakutakia utekelezaji mwema.



ILALA V. NYEMBEKE
MKUU WA SHULE
+255 787 086 205

FORMA

SHULE YA SEKONDARI MWEGA FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI NA KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA

**Picha 2 ziletwe
shuleni**

1. TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

Jina kamili la mwanafunzi.....
Tarehe ya kuzaliwa:
Mahali alipozaliwa: Mkoa Wilaya
Unaishi wapi? Kata Kijiji
Uraia
Shule uliyotoka:
Nambari ya mtihani :PS

2. TAARIFA YA MZAZI/MLEZI

Jina la mzazi/mlezi
Kazi ya mzazi/mlezi
Anuani ya mzazi/mlezi
Simu ya mzazi/mlezi

3. TAMKO LA MWANAFUNZI:

Mimi Nimesoma na kuyaelewa maelekezo na taratibu zote zilizotolewa. Hivyo nakubali/sikubali kuipokea nafasi niliyopewa.

Sahihi yangu: Tarehe

4. TAMKO LA MZAZI/MLEZI:

Mimi nakubali /sikubali nafasi hii aliyopewa mwanangu baada ya kusoma na kuelewa taratibu zote za shule kama zilivyoainishwa kwenye barua yako yenye Kumb. Na. MWG/SS/REG/2021/01

Sahihi yangu Tarehe

5. TAMKO LA MWENYEKITI WA MTAAL/KITONGOJI/KIJINI:

Ninathibitisha/sithibitishi kuwa taarifa zote zilizotolewa na mzazi na Mwanafunzi ni sahihi/si sahihi kuwa ni wakazi/si wakazi wa eneo langu. Nami kwa niaba ya serikali naahidi kushirikiana na Uongozi wa shule kuhakikisha Mwanafunzi anahudhuria vipindi vyta masomo shuleni kwa muda wote.

.....
Jina la Mwenyekiti wa Mtaa/Kitongoji/Kijini

.....
Sahihi

Tarehe.....

Kata isiyohusika

FORM B**MWEGA SECONDARY SCHOOL
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

From: The Medical Officer

To: The Headmaster

Mwega secondary school
P.O.Box 99,
Mikumi.

RE: MEDICAL CERTIFICATE FORM

(To be completed by Medical Officer)

I have examined, who inspires to
Join Form One at your school as follows:-

AREA.**REMARKS.**

- | | |
|-------------------|-------|
| 1 Skin | |
| 2. Eye | |
| 3. Ear | |
| 4. Teeth | |
| 5. Chest | |
| 6. Spleen | |
| 7. Abdomen | |
| 8. Urine | |
| 9. Stool | |
| 10. HB Hemoglobin | |
| 11. Meningitis | |
| 12. Sickle cell | |
| 13. Asthma | |
| 14. Pregnancy | |

ADDITIONAL INFORMATION. e.g. Physical defects or impairments infections
Chronic or family diseases etc.

I certify that the above student is fit/unfit for admission.

Signature.....

Designation.....

Station.....

Date.....

Official stamp.....